



BODI YA KAHAWA TANZANIA

TANGAZO

UFUNGUZI WA MSIMU WA KAHAWA 2018/2019

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Kahawa Tanzania anapenda kuwatangazia ufunguzi wa msimu mpya wa kahawa kwa mwaka 2018/2019. Tarehe za ufunguzi kwa Kanda ni kama ifuatavyo;

Na.	Kanda	Mkoa	Tarehe ya Ufunguzi
1.	Kaskazini	Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Morogoro, Tanga	1 Juni, 2018
2.	Mbeya	Mbeya, Katavi	1 Mei, 2018
3.	Kigoma	Kigoma	1 Mei, 2018
4.	Mara	Mara, Mwanza, Geita	1 Mei, 2018
5.	Kagera	Kagera	1 Mei, 2018
6.	Ruvuma	Ruvuma, Iringa, Njombe	15 Juni, 2018

Mambo muhimu ya kuzingatia:

1. Kama ilivyokwisha elekezwa na Serikali, Bodi ya Kahawa haitatoa leseni za ununuzi wa kahawa kwa makampuni binafsi kununua kahawa vijijini. Makampuni binafsi yatanunua kahawa kwenye mnada wa kahawa.
2. Makampuni yaliyokuwa yananunua kahawa vijijini yanatakiwa kukamilisha taratibu za kuomba leseni za kununua kahawa kwenye mnada wa kahawa.
3. Maombi ya leseni mpya kwa wanunuzi wa kahawa mnadani na wale wanaobadilisha leseni zao za awali yaletwe kwa Mkurugenzi Mkuu kwa anuani iliyoko hapa chini.
4. Vyama vya ushirika vinatakiwa kuanza kukusanya kahawa kutoka kwa wakulima mara tu inapokuwa tayari na kuipeleka kwenye viwanda vya kukobolea kahawa ili kuharakisha zoezi la uuzaji wa kahawa za Wakulima
5. Vyama vya msingi vitakavyouza kahawa mnadani vitaomba vibali kwa kujaza fomu Na. TCB/FG/001 zinazopatikana kwenye ofisi za Kanda za Bodi ya Kahawa Tanzania au kwenye tovuti ya Bodi ya Kahawa Tanzania.

6. Kama ilivyoelekezwa viwanda vyote vya kukoboa kahawa vikamilishe taratibu za kujisajili kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani kabla ya tarehe 30 Mei 2018.
7. Makampuni yatakayotoa huduma kwa vyama vya ushirika (usafirishaji, ukoboaji, magunia n.k), kukodisha miundo mbinu yao (CPU) na taasisi za fedha zitakazotoa mitaji kwa vyama vya ushirika na kutaka kuingia mikataba na Bodi kwa ajili ya kukusanya fedha zao wafanye hivyo kabla ya tarehe 15 Juni, 2018.
8. Bodi ya kahawa itaaza mara moja kuendesha minada ya kahawa pindi kiasi cha kutosha (stocks) zitakapokuwa tayari.
9. Halmashauri za wilaya zihakikishe kuwa CPU zote zilizoko katika maeneo yao zinatumika na zinafunguliwa mara tu kahawa inapokuwa tayari ili kufanikisha lengo la Serikali la kuongeza ubora wa kahawa.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Bodi ya Kahawa Tanzania
S.L.P. 732 – Moshi
Simu: 027-27-52324
Nukushi: 027-27-52026
Barua pepe: info@coffeeboard.or.tz
Tovuti: www.coffeeboard.or.tz